
# CHOZI LA DAMU

Bernard Mukasa






2.Oh kila siku tunapolala baba zetu hamjarudi;
Asubuhi tukiamka baba zetu mmeondoka.
Siku tukibahatika kushtuka usiku wa giza,
tunachokishuhudia ni mama anapigwa makofi;
Na vitisho vya talaka, matusi, na harufu ya pombe,
Darasa gani mnatupa watoto wenu.

3.Oh tukirudi toka shuleni; madaftari hamkagui,
eti kwa kuwa tumechoka burudani mwatuwekea.
Video mnazowasha picha za vita na mauaji,
au mikanda iliyorekodiwa Sodoma Gomola.
Hamkumbuki yakuwa mnayafuta ya darasani;
Urithi gani mnatupa wazazi wetu.

4.Oh kwenye chakula cha usiku, siku zote baba hayupo,
kusali sala za pamoja kwenye nyumba yetu ni mwiko;
Anachelewa kutoka kwa mama mdogo yule wa siri,
Au giza likizidi hatarudi mpaka Asubuhi.
Na mama akishajua mbio kwa 'Anko' wa usiseme;
Familia moja baba na mama watano.

5.Oh kwasababu ya mambo haya ndugu zetu wanaumia,
wapo wanaorandaranda mitaani bila makazi;
Wengi wamelazimika kuajiriwa bado wadogo,
hawana tena nafasi ya kusoma wapate elimu.
Na wengi wanajiuza miili yao ili waishi,
mbona dunia umetugeuka watoto.